BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Tano – Tarehe 29 Novemba, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

II. MASWALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

14. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa maslahi ya Walimu ni duni na kwa kuwa wakati wa Serikali iliyoongozwa na Marehemu Mzee Idrisa Abdul Wakil, mshahara wa mwalimu ulikuwa ndio mshahara mkubwa miongoni mwa watumishi wa Umma nchini. Na kwa kuwa hivi sasa hali hiyo haipo tena.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mishahara na stahiki nyengine za walimu wetu nchini, ili kurejesha hali iliyokuwepo wakati huo.

94. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tuna tatizo la walimu katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba na hivi sasa tukiangalia sana kwa ujumla tunaona idadi ya walimu ni wengi lakini ukiangalia skuli za shamba walimu ni kidogo, na wanaotakiwa hivi sasa ni wa sayansi tu.

Je, Wizara imejipanga vipi kuajiri walimu wa masomo mengine.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira :

53. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Kutokana na umuhimu wa maji katika maisha ya binaadamu, na usumbufu unaopatikana katika suala hili la Maji, hasa katika vijiji vyote vya Jimbo la Nungwi, ambao pamoja na kuchimbwa visima zaidi ya vitano katika Jimbo hili, lakini bado maji ni kikwazo katika Jimbo hili na maeneo mengi ya Wilaya ya Kaskazini ‘A’ Unguja.

Je, Serikali imejipangaje katika kuirejesha huduma hii ya maji kwa kupitia kisima kikuu cha enzi (Kiwashange) kwa kusambaza maji

mengi na safi katika maeneo yote ya Wilaya za Kaskazini ‘A’ Unguja.

57. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Hivi karibuni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, ilipokea msaada wa jumla ya Shs. 92 bilioni, kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji hapa Zanzibar, Unguja na Pemba.

Kwa kuwa Zanzibar tuna Majimbo Hamsini na Nne (54), Je, Mhe. Waziri haoni umefika wakati wa kuzitumia fedha hizo kwa kila Jimbo Bilioni moja (1) kwa ajili ya kushughulikia na kuondoa kabisa tatizo la maji hapa nchini.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

136. MHESHIMIWA. SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Itakumbukwa kwamba katika maadhimisho ya Mei mosi yaliyofanyika Makonyo Pemba tarehe 1/5/2015, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma aliahidi kuanzishwa kwa kitengo cha usuluhishi wa migogoro ya kazi upande wa Pemba katika Bajeti ya 2015/16.

a) Ni sababu gani iliyopelekea kutotimizwa kwa ahadi hiyo.

b) Serikali inasemaje juu ya utekelezaji wa ahadi hiyo ili kuwapunguzia usumbufu wafanyakazi waliopo Pemba kufuata huduma hizo Unguja.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

4. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Zao la karafuu ni zao ambalo linaingiza mapato mengi sana katika nchi yetu na muitikio wa wananchi katika kuimarisha zao hili ni mkubwa, na hivyo mahitaji ya miche ya mikarafuu yanaongezeka siku hadi siku.

a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza miche ya mikarafuu ambayo itaenda sambamba na mahitaji ya wakulima kwa mwaka.

b) Je, ni miche mingapi ya mikarafuu iliyopo kwenye vitalu vyake kwa sasa na Je, anadhani itakidhi mahitaji ya wakulima waliopo.

c) Je, Wizara yake imeshafanya utafiti kubaini tatizo hilo na imeshawapatia elimu wakulima ili kuepukana na tatizo la kufa kwa baadhi ya miche baada ya kupandwa.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

62. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID MOHAMMED (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kwa kuanzisha Idara ya Usafirishaji. Hata hivyo kuanzia tarehe 1/7/2016 mpaka tarehe 8/7/2016 kulikuwa na upungufu mkubwa sana wa fomu za kupasishia magari katika Idara hiyo.

a) Ni sababu gani iliyosababisha kutokea kwa upungufu huo.

b) Hatua gani zilizochukuliwa kuzuwia upungufu huo usitokee tena.

65. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inakusanya mapato mengi sana Tanzania nzima ikiwemo Zanzibar katika utumiaji wa simu ambazo zimeenea hata vijijini kote hapa Zanzibar.

Je, Serikali ya Zanzibar inafaidika vipi na mapato hayo ambayo hata wananchi wanyonge wa Zanzibar wanayachangia.

75. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Abiria kutoka Unguja au Pemba wanaosafiri kwa njia ya bandari zetu, hupita bandarini hapo bila ya upekuzi wa mizigo yao, na kuhakikisha kuwa ni salama bila ya matatizo.

Kwa kuwa hivi sasa hali ya uaminifu duniani si nzuri, Je, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha upekuzi wa mizigo na abiria wanaosafiri baina Unguja na Pemba ili kuhakikisha usalama wa mizigo yao.

Wizara ya Afya:

11. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wagonjwa wa tezidume wamekuwa wakisumbuka muda mrefu kusubiri majibu ya vipimo na kubakia bila matibabu, hata wengine hulazimika kufuata matibabu nje ya nchi.

a) Je, ni sababu gani zinazopelekea wagonjwa kuchukuliwa damu na kwend
b) a kufanyiwa uchunguzi nje ya nchi wakati muelekeo wetu ni Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa.

b) Je, Kitendo cha wagonjwa kukaa muda mrefu wakisubiri matokeo ya vipimo bila ya kupata tiba, tunaokoa maisha yao au tunachangia maisha yao yapotee.

c) Kuna wagonjwa tangu mwaka jana wamechukuliwa vipimo mpaka sasa matokeo hawajayapata na mmojawapo amelazimika kutibiwa Nairobi na mpaka anarudi Aprili, 2016 matokeo yake bado hayajarudi, nini tatizo.

32. MHESHIMIWA ALI KHAMIS BAKARI (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni kwa kiasi gani elimu ya TB imetolewa kwa jamii hasa kwa kuzingatia kuwa wagonjwa kabla hawajahudhuria Hospitali, wanapaswa kujilinda ili wasiwaambukize watu wengine.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

149. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Kwa kuwa Serikali imejenga Hoteli ya Uwanja wa Amani na kwa kuwa hoteli hiyo imepoteza hadhi yake licha ya kuwa ni hoteli ya zamani.

Je, Hoteli hiyo inamilikiwa na nani hivi sasa.

III. HOJA ZA SERIKALI

Waziri wa Fedha na Mipango:

Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo. – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
29 Novemba, 2016.

(Amour M. Amour)
KNY. KATIBU